

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI MAMLAKA YA UWEKEZAJI NA MAENEO MAALUMU YA KIUCHUMI TANZANIA (TISEZA)

Simu Na: (255) 22 2116328-29,  
Nukushi: (255) 22 211 8253,  
Barua pepe: [info@tiseza.go.tz](mailto:info@tiseza.go.tz)  
Tovuti: [www.tiseza.go.tz](http://www.tiseza.go.tz)



PSSSF - Jengo la Golden Jubilee,  
Ghorofa ya kwanza, Wing A  
S.L.P 938,  
DAR ES SALAAM.

---

**Unapojibu tafadhali taja:**

**Kumb. Na. CB.48/259/01A/77**

**11 Februari, 2026**

Mkurugenzi wa Halmashauri,  
Mji wa Kibaha,  
S.L.P 30153 ,  
**PWANI**  
[td.kibaha@pwani.go.tz](mailto:td.kibaha@pwani.go.tz)

**YAH: KUOMBA UTHIBITISHO WA UMILIKI WA VIWANJA NAMBA 265 KITALU 'A'**  
**VILIVYOPO ENEO LA VIWANDA LA MISUGUSUGU MIOMBONI.**

Kichwa cha habari hapo juu cha husika.

2. **Tanzabread Company Limited** ni mwekezaji aliyesajiliwa na Mamlaka ya Uwekezaji na Maeneo Maalum ya Kiuchumi Tanzania (TISEZA) kwa ajili ya mradi wa kuandaa chakula (Food processing). Mwekezaji huyu alipatiwa cheti Namba 202542682 kilichotolewa tarehe 14 Aprili, 2025. Mwekezaji huyu amenunua kiwanja namba 265 Kitalu 'A' kilichopo eneo la viwanda la Misugusugu, katika Mji wa Kibaha, Mkoa wa Pwani. Kampuni imewasilisha mkataba wa mauziano ya kiwanja husika kati ya Jurijs Anatolijs Martinovs (Muuzaji) na Tanzabread Company Limited (Mnunuzi).

3. Ili Mamlaka iweze kuendelea na taratibu za kuhuisha taarifa za mradi husika, na kwa kuzingatia kuwa eneo hili limenunuliwa na kampuni yenye umiliki wa kigeni, tunaomba ofisi yako itoe uthibitisho wa kutambua mauziano hayo, hali ya umiliki wa sasa pamoja na matumizi halali ya eneo hilo.

Nashukuru kwa ushirikiano.



M.D.Mdanya

Kny: **MKURUGENZI MKUU**

**Nakala:** Mkurugenzi,  
Tanzabread Company Limited  
S.L.P 78570,  
**DAR ES SALAAM**